

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**RATIBA YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE
(STANDARD FOUR NATIONAL ASSESSMENT-SFNA)**

NOVEMBA 2017

TAREHE NA SIKU	MUDA (SAA)	NAMBA MFICHO	SOMO
22.11.2017 JUMATANO	2:00 – 3:00	02	ENGLISH LANGUAGE
	3:00 – 4:00		MAPUMZIKO
	4:00 – 5:30	04	HISABATI
		04E	MATHEMATICS
	5:30 – 7:30		MAPUMZIKO
	7:30 – 8:30	05	SAYANSI
		05E	SCIENCE
<hr/> <hr/>			
23.11.2017 ALHAMISI	2:00 – 3:00	01	KISWAHILI
	3:00 – 4:00		MAPUMZIKO
	4:00 – 5:00	03	MAARIFA YA JAMII
		03E	SOCIAL STUDIES

	5:00 – 7:00		MAPUMZIKO
	7:00 – 8:00	06 06E	STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO VOCATIONAL SKILLS, PERSONALITY DEVELOPMENT AND SPORTS
	8:00 – 9:00		MAPUMZIKO
	9:00 – 10:00	07 07E	TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) INFORMATION AND COMMUNICATION TECHNOLOGY (ICT)

MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Upimaji wa mwaka 2017** iliyoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenye maswali ya upimaji, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Upimaji**.
3. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo ndani ya Karatasi ya Upimaji na Ratiba ya Upimaji**, **maelekezo yaliyomo katika karatasi ya upimaji husika ndiyo yatakayofuatwa**.
4. Watahiniwa **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa upimaji **wote** isipokuwa **DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa somo la **Hisabati**.
5. Msimamizi wa watahiniwa **WASIOONA** awe mtaalamu mwaminifu aliye na **uwezo wa kusoma maandishi na alama za 'Braille'**.
6. Watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za upimaji na za kujibia zenye **maandishi yaliyokuzwa**, zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.
7. Karatasi zenye majibu ya watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** zifungwe kwenye **bahasha za pekee**. Zisichanganywe na karatasi za watahiniwa wenye Uoni wa kawaida.
8. Watahiniwa waelekezwe;
 - (a) Kuingia ndani ya chumba cha upimaji nusu saa kabla ya muda wa upimaji na watakochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya upimaji kuanza hawataruhusiwa.
 - (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa upimaji.
 - (c) Kuandika jina kamili na namba ya upimaji kwa usahihi.
 - (d) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina ya watahiniwa. Ikiwa mtahiniwa ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa upimaji.
 - (e) Wakijihusisha katika udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya upimaji.